

Tegua Farasi Wako! **Yoshua 11:6**

Moja ya maudhui makuu ya Biblia ni tumaini. Kumtumaini Mungu. Weka imani yako kwake. Mwegemee Yeye. Yeye pekee ndiye tabibu mkuu. Yeye pekee aweza kukukamilisha. Yeye pekee aweza kukuokoa. Hata hivyo, tangu hapo kale, wanadamu wametafuta sababu fulani fulani ili kuweka imani zao na matumaini katika vingine au watu wengine.

Katika Yoshua 11, shirikisho lililokuwa chini ya mfalme wa Hazori, liliungana ili kulishambulia jeshi changa la Mungu. Kwa mujibu wa wanahistoria wa kiyahudi, vikosi vya ardhini vyenye askari wapatao 300,000, magari ya kuvutwa na farasi 20,000 na askari waliopanda farasi wapatao 10,000 walijitokeza ili kupigana na Yoshua. Idadi hii imeelezwa kama “watu wengi mno kama mchanga ulio ufuoni mwa bahari,” Yoshua 11:4.

Bila kujali jeshi la maadui lilionekana ni kubwa kiasi gani; Mungu alimuahidi Yoshua kuwa angelitia hili jeshi la adui katika mikono yake. Na Mungu alimwamuru Yoshua kwamba farasi watakaowateka nyara “wawategue”. Kumtegua farasi kwa kifupi humaanisha hatua ya kumtia kilema huyu mnyama. Kwa nini Mungu, hakutaka Israeli wamiliki farasi kwa ajili ya vita? Ni kwa sababu Mungu alijua kwamba ili taifa liokolewe, lazima wajifunze kumtumaini Yeye. Kwa hiyo Mungu alitaka awe ndiye ukuta wa moto unaoizunguka Israeli, na aliwataka wamtumaini Yeye kabisa kwa ulinzi na katika yote, wamtumaini Yeye kabisa kabisa kwa ajili ya wokovu wao wa muda na wa milele. Hivyo, Mungu aliwaamuru Israeli kuwa kwa ajili ya ulinzi, wokovu, na uhuru wasivitumainie vinavyoonekana. Kwa kujua kuwa kama angewaacha wavitumainie vitu, wangeanza kuvimba kichwa au wangetumainia mali zao na kumwacha aliye chanzo cha nguvu, ambaye NIKO.

Katika Zaburi 20:7 Daudi alisema, “Hawa wanataja magari na hawa farasi, bali sisi tutalitaja Jina la BWANA, Mungu wetu.” Na siku hizi wengi hutumaini; pesa, mali, madaraka, umaarufu, bahati, kiburi, vitabu, jamii, soko la hisa, vyama vya kisiasa na mengineyo. Hata hivyo, uhalisia ni kwamba, yupo tabibu Mkuu mmoja. Kuna mwokozi mmoja. Kuna Bwana mmoja. Ndiye na Yeye pekee aweza kuokoa leo. Hivyo, “tegua farasi wako” na umwegemee Yeye.

Tafadhari zingatia mistari hii kuhusiana na kumtumainia Mungu;

2 Samueli 7:28 Na sasa, Ee Bwana MUNGU, wewe ndiwe Mungu, na maneno yako ndiyo kweli, nawe umemwahidia mtumwa wako.

Zaburi 13:5 Nami nimezitumainia fadhili zako; Moyo wangu na uufurahie wokovu wako.

Zaburi 25:1-3 Ee BWANA, nakuinulia nafsi yangu, Ee Mungu wangu, Nimekutumaini Wewe, nisiaibike, Adui zangu wasifurahi kwa kunishinda. Naam, wakungojao hawataaibika, wataaibika watendao uhaini bila sababu.

Zaburi 31:14 Lakini mimi nakutumaini Wewe, BWANA, nimesema, Wewe ndiwe Mungu wangu.

Zaburi 52:8 Bali mimi ni kama mzeituni umeao katika nyumba ya Mungu. Nazitumainia fadhili za Mungu milele na milele.

Zaburi 118:8 Ni heri kumkimbilia BWANA kuliko kuwatumainia wanadamu.

Isaya 2:22 Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi yake i katika mianzi ya pua yake; kwa maana hudhaniwae kuwa ni kitu?

Isaya 12:2 Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu, nitatumaini wala sitaogopa.

Yohana 14:1 Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.

Warumi 9:33 Kama ilivyoandikwa, Tazama, naweka katika sayuni jiwe likwazalo, na mwamba uangushao; Na kila amwaminiye hatatahayarika.